**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA KILIMO**

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA NAFAKA NA MAZAO MCHANGANYIKO**

**Kumb. Na. AB. 77/325/01/6** **14 Mei, 2025**

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA) anawatangazia watanzania wote wenye sifa na nia ya kufanya kazi ya udereva kutuma maombi ya kazi kwa nafasi kumi na nne (14) za kuajiri madereva kwa mkataba.

### 1.0 DEREVA - NAFASI 14

### 1.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Mwombaji awe na Cheti cha Kidato cha Nne (Form IV) na Leseni ya Daraja E au C ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua miaka mitano bila kusababisha ajali. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya Ufundi Stadi (VETA), Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali. Mwombaji aliyesomea Cheti cha Huduma ya Magari ya Umma ‘’Public Service Vehicle (PSV)’’ maombi yake yatapewa kipaumbele.

### 1.2 KAZI NA MAJUKU

i) Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari;
ii) Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi;
iii) Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari;
iv) Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali;
v) Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari;
vi) Kufanya usafi wa gari; na
vii) Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na Msimamizi wake.

### 1.3 NGAZI YA MSHAHARA

Waombaji watakaopata nafasi na kupewa mkataba wa kazi watalipwa mshahara ambao ni asilimia themanini na tatu nukta nne (83.4%) ya mshahara wa madereva kwa mujibu wa muundo wa kada ya madereva wa COPRA.

**MASHARTI YA JUMLA**

1. Awe Raia wa Tanzania
2. Awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi umri wa miaka 45
3. Asiwe Mwajiriwa wa Serikali
4. Awe tayari kupangiwa kituo cha kazi popote mwajiri atakapompangia
5. Kila mwombaji aambatishe nakala ya cheti cha kuzaliwa, kitambulisho cha taifa au namba ya utambulisho wa taifa (NIDA)
6. Waombaji wote waambatanishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza (Detail Curriculum Vitae) yenye anuani inayotumika, namba za simu zinazopatikana na Anuani ya Barua pepe (E-mail address) pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika;
7. Kila mwombaji aambatishe barua au cheti (certificate of Service) kutoka kwa mwajiri wake wa zamani kuthibitisha utendaji wake wa kazi;
8. “Testmonial” “Provisional Results” Statement of result hati ya matokeo ya kidato cha Nne na kidato cha Sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA;
9. Awe na barua ya utambulisho kutoka kwa mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa
10. Waombaji waliosoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na vimethibitishwa na Mamlaka husika (TCU, NECTA na NACTE);
11. Waombaji kutoka Mikoa ifuatayo watapewa kipaumbele; Katavi, Tabora, Mwanza, Kagera, Simuyu, Singida, Kilimanjaro, Manyara, Morogoro, Dar es Salaam, Mtwara, Ruvuma, Njombe na Mbeya
13. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **23 Mei, 2025**

**Muhimu: Maombi yatumwe kwa njia ya posta au kwa mkono katika Ofisi za Mamlaka zilizopo Dodoma, Mtaa wa Njedengwa, Jengo la Kahawa . Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu kwenye anuani ya barua ielekezwe kwa ;**

**MKURUGENZI MKUU,**
**MAMLAKA YA UDHIBITI WA NAFAKA NA MAZAO MCHANGANYIKO (COPRA),**
**S.L.P 2780,**
**DODOMA.**